LIBRARY FB ATTORNEYS

TANGAZO LA SERIKALI NA. 372 la tarehe 20/11/2026

SHERIA YA BENKIKUU YA TANZANIA,
(SURAYA 197)

_____

KANUNI

_____

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 70)
KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MATUMIZI YA FEDHA ZA KIGENI ZA MWAKA 2026

Jina
TS. Na. 198 la 2025

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2026 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025 ambazo hapa zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho yakanuni ya 4

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 4-

(a) kwa kufuta maneno "baada ya mashauriano na Gavana"; na

(b) kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo ifuatayo:

"(3) Kanuni hizi hazitatumika kwa mkataba wa bidhaa au huduma unaohusisha muamala unaovuka mpaka wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Kigeni.".

Sura ya 271

Kuongeza kanuni ya 6

3. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 5, kanuni mpya ifuatayo:

"Kamati ya ushauri

pale **6**. Waziri anaweza, itakapohitajika, kuunda kamati ya ushauri kwa ajili ya kuchambua na kumshauri kuhusu masuala yanayohusu utekelezaji wa Kanuni hizi.".

4. Kanuni kuu zinarekebishwa kwenye Jedwali-

LIBRARY FB ATTORNEYS

Marekebisho ya Jedwali

(a) katika kipengele Na. 2 kwa kuongeza maneno “yanayotambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kinga na Haki za Kidiplomasia na Kibalozi, Sura ya 356” baada ya neno “nchini”;

(b) katika kipengele Na. 4 kwa kuongeza maneno “yaliyomo ndani ya viwanja vya ndege” mara baada ya neno “ushuru”;

(c) kwa kuongeza mara baada ya kipengele Na. 4, vipengere vifuatavyo:

“

5.	Malipoyanayotokana na makubaliano ambayoSerikali imeingia naambayoyameidhinishwa na Baraza la Mawaziri.
6.	Miamala inayohusisha malipo ya bima mtawanyo kwa kampuni zabima zanje ya nchi.
7.	Miamala inayofanywa na mwendeshaji wa utalii ambaye ni mkazi wakati wa kulipia bidhaa au huduma za utalii kwa niaba ya mtalii kutoka nje ya nchi.

”

Dodoma,
17 Novemba, 2026

KHAMIS MUSSA OMAR
Waziri wa Fedha